Kwako bibi

Suruali imeruhusiwa tena ?

Kufuatana na mila za mababu yetu,mavazi ina maana yake ya kutambulisha tafauti kati ya mume na mke. Tangu zamani ilikuwa vile na wote wawili walikuwa wakivaa namna mbalimbali.

Kizungu kilipo tufikia, wanawake, pia na wanaume wamoja wamoja wakaanza kufuata kikondoo namna ya kuvaa ya wakoloni. Ndipo tuliona baba zetu kusokota kamba shingoni na kutiako koti (cravate, veste). Bila hiyo,hawangaliweza kuitwa wasirimu (évolués, civilisés).

Wakati huo,kulikuwa hata kaka zetu waliosomea ulaya waliopenda sana kuitwa wa "Belgicains". Nguo zao zilikuwa koti za kila aina ya "trois pièces" na hata mashati yenyi sura ya vizibao.

Dada zetu nao pamoja na wale wamama wasirimu,walikuwa wakivaa makabana ao kanzu fupi yenye kuonya mapaja na hata nguo za ndani kama silipe na vivihivi. Waliita nguo hizo "mini-jupe", "mini-robe", "tremblant". Hiyo yote ilikuwa kufuata kikondoo tabia za wakoloni zisizo tabia za mababu zetu.

Ni hapo baba wa Taifa alifungua macho na kutangaza mbele ya ulimwengu chama kiitwacho "authenticité", kilichowakataza wanachama wote kuvaa hizo nguo za wazungu zenyi kufezeesha tabia zetu za kiafrika. Aliwalazimisha wazairwa wote kuvaa mavazi ya kikwetu kama vile "abacost" kwa wanaume na vikwembe kwa wanawake. Hakukosa kuwakabizi wasichana na wamama wote kuacha rangi za midomo,nyele za singa na vivihivi.

Tunasangaa saana kuona wadada wengi hawashiki kanuni za nchi hata wale waliosoma. Ukiwauliza sababu gani wavaa kanzu fupi hujibu eti "njo la mode, haifai kujiachilia,inafaa kurudia mtoto". Na ni hasa wa bibi na wenyimali,ao watoto wawakubwa wenyi kuvaa mavazi hiyo. Eti ndio wasifanane na wengine wamaskini. Hiyo yote mbele ya mabwana zao ao wazazi wao wenyi kuongoza nchi yetu.

Ewe dada zetu, hiyo ndio namna ya kuonyesha maendeleo ya nchi yetu? Mbona muko munarudi nyuma bila kujuwa ?

Kwa kumaliza, twakumbusha kila dada na mama hao wanaopevuka kama katika asili yetu suruali "pantalon" ni vazi za wanaume na mabwana. Anayejitaidi kuivaa ndio kusema anahitaji kugeuka naye bwana nyumbani kwake. Kina mama angalisho. Kwani wangwana husema kama kinwa cha mzee kinanuka lakini hakisemi uongo. Hiyo tabia ya kuvaa suruali na ya kuonya silipe kwa wapitanjia yaweza kuleta hasara. Alamsiki.

Bujiriri Mwangaza

Kwa kupiganisha " Kolera " yafaa kutumia maji safi

Leo tena tumepokea ofisini mwetu, maandishi ya ndugu Lugunga ambaye aendelea siku hizi kujielimisha katika cho cha majifunzo ya upashaji wa habari (ISTI) huko Kinshasa.

Maandishi yake ambayo twachapa katika mistari ifuatavyo yahusu usafi wa maji kusudi ya kujikinga kwa magonjwa mengi hasa zaidi ile ya kipindupindu ama kolera.

Nilipigwa na bumbuazi (msangao, étonnement) niliposoma katika magazeti ya kwamba ugonjwa wa kipindupindu (kolera) waangamiza raia huko Bukavu. Wengi husema kama ni bahati mbaya kushikwa na ugonjwa kama ule na wengine hueleza kuwa ni ugonjwa wa maskini na wakosefu.

Jambo muhimu katika manongonezo hayo ni kujikinga tu kwa ugonjwa kama ule tukichungua kwa makimu maji tunayotumia kwa kunywa, kufua na hata kunawa. Maji hayo yaweza kuwa mabaya na kufikia hata kuondoa mtu maisha. Idadi ya watu wanaotumia maji yasiyo safi ni wengi sana siyo tu katika sehemu ya vijiji bali pia ;katika miji mikubwa. Kuna wakati watu wanayatumia maji hayo machafu kwani hawafahamu kanuni za afya. Shida kuu ni ile ya kujua ni maji gani yaliyo safi yale yaliyo machafu.

Inaaminika kuwa maji ya mifereji, yale ya mito na maziwa ni yenyi uchafu mwingi. Yule anayekunywa maji hayo anaingiza mikrobi mwilini mwake. Mikrobi ambayo ni msinji wa magonjwa mengi. Maji safi kama vile waalimu hutufundisha mashuleni, yatoka katika visima. Kwani hayo ni maji ya mvua yanayotoka udongoni na yenyi kukuchujwa (filtrer) wakati yanapopenya katika udongo.

Tunapotumia vyombo vyeni uchafu, kama vile vibuyu visivyosukuliwa ao tukiwaacha wanyama wazunguuke ovyo pembeni ya visima twaweza kuchafua pia maji [yetu ya kunywa.

Alama ya kwanza mtu anapopatwa na ugonjwa ambao msinji wake ni maji machafu ni kule kuhara. Vipimo vya waganga vyaonyesha wazi kuwa magonjwa kama vile "amibioses", "typhoïde" ambayo yaleta uzaifu mwilini na hata kumuambukia yeyote anayemkaribia mgonjwa, hatuwezi pia kusahau "poliomyélite" ambao wapoleza viwiliwili na mgonjwa na hata kufikia kumletea ulemavu. Yatokana na kunywa maji machafu.

Maji machafu yaleta hata michango tumboni (nyoka) kama vile ascaris, tenia, amibe ...

Kwa kujikinga siyo tu kuchanjwa dawa za kolera, bali pia kuchagua maji tunayotumia. Yafaa hasa kuchemsha maji mbele ya kuyanywa. Jambo hili lawahusu hasa wale wanaotumia maji ya mabomba ya shirika linalohusika na ugawaji wa maji ama REGIDESO. Maji hayo si safi. Redio, televisheni na magazeti vyatoa mashauri lakini watu wengi hawapendi kusikia kuwa katika maji hayo mwapanga mikrobi inayoweza kutuletea hasara kubwa. Zaidi ya hayo, yafaa pia kulinda vema visima tunavyotumia. Kwani ugonjwa wa kipindupindu watokana hasa na UCHAFU. Uchafu wa maji na ule wa vyombo tunavyotumia. Kila mtu ajihimize kutia usafi nyumbani kwake.

Viongozi nao waunge raia mkono kwa kuomba shirika REGIDESO katika harakati za kutoa maji safi ili sisi wote kwa jumla tuishi kwa usalama. Tupate pia kusema kama wangwana : "allah, apitishe mbali balaa hilo". Tusisahau pia kunawa mikono kwa sabuni mbele ya kula ao kisha kwenda chooni. Pia tuache kula ovyo ovyo chakula kibichi kama muwa, chungwa, embe ...

LUBUNGA B. M'KYOBA

JUA

Gazeti la Kivu

Uhusiano kati ya China na Zaïre wadumishwa

Ni tangu sasa siku nyingi nchi za China na Zaïre zajitatanua kudumisha uhusiano wao katika mambo yenyi kuelekea siasa, uchumi wa kiaskari. Na kutokana na hali hiyo bora ya uhusiano,wajumbe kazaa wa kazaa wa nchi hizo mbili rafiki wakutana mara kwa mara ili kuchungua kwa karibu matunda ya uhusiano wao na ginsi gani kuuimarisha siku za usoni.

Ni hivi tangu siku ya posho tarehe 19 Januari 1985, ujumbe moja maalum wenyi kuundwa na wabunge 12 wa nchi ya China katembelea nchini Zaïre ili kujionea wenyewe namna gani Zaïre yasonga mbele katika maendeleo yake kutokana na mashauri yanayotolewa na wajuzi toka China.

Baada ya kufika Kinshasa,mji mkuu wa Zaïre,wabunge hao walipokelewa katika masimulizi rasmi na wananchi Kititwa, makamu wa kwanza wa Prezidenti wa Chama cha Mapinduzi MPR, Mpinga, katibu imara wa Chumba cha Siasa, Prezidenti wa Bunge kuu la Taifa (halmashauri), na wenginepo wa Serikali,wageni hao wa heshima walitembelea kituo cha moto wa stimu cha Inga, ulalo Mareshali Mobutu na Bustani ya mimea mbalimbali ya mji wa Kisantu katika jimbo la Zaïre ya Chini, kiwanda cha uchimbaji wa madini ya shaba (cuivre) mjini Kamoto na mahali kazaa muhimu wa miji ya Lubumbashi na Kolwezi (jimboni mwa Shaba) na Shamba la wanyama la Virunga (jimboni mwa Kivu).

Bisimwa Tserou

BUMBUAZI !

Habari za mbuu

Uwizi, ujambazi na kazalika waangamiza wakaaji wa Chiriri usiku na mchana. Ebu mumesahau malaria na kipindupindu (Kolera).

Kwa kweli wao hushambulia sasa na mnuko wa uchafu na maji toka choo cha hospitali ya mganga "R...". Kwa kuwa shimo hilo mambo hayo yaporomokeamo lipo wazi. Kutokana na hali hiyo, mbu nazo huzaana na kuwasakanya wakaaji kama ndege za vita. Hatari zaidi: Baada ya ugonjwa wa malaria wenyi kuletwa na mbuu, nzi nazo zitapata ginsi yakuleta viini (mikrobi) na kuleta ugonjwa wa kipindupindu.

KINSHASA ITAPOKEA SEMINA YA WAHUBIRI WA KIPROTESTANTI

Mkutano mkubwa wa makanisa ya kiprotestanti utafanyika tangu tarehe 7 hadi 14 mwezi wa nne ujao. Watakao kusanyika mjini Kinshasa wahubiri kutoka majimbo yote,makanisa (communautés) yote pamoja wahubiri wa kiaskari na wale wa wanawake.

Tangazo moja la "ECZ" (Eglise du Christ au Zaïre) lilifahamisha kama shabaa la mkutano huo ni ya kuamsha kampeni za kutangaza neno la Mungu katika Zaïre nzima. Wakuu wa kanisa la kiprotestanti watajipatia nafasi,wakati huo,ili kuchunguza yote waliokwisha tenda ahadi sasa, kwani kanisa hilo limetimiza hapo majuzi miaka 100 ya kazi nchini humu. Watachunguza pia yale yanayoitaji marekebisho (corrections). Na baadaye watachukua mipango mipya juu ya kuendelesha kazi yao katika kila jimbo la kila kanisa.

Kwa upande mwengine,semina ya wachungaji wamakanisa pamoja na wake zao ilifunguliwa mjini Kinshasa.

Lubunga Bya'ombe